

JobORTUNITY

Be the right you for the right job



Kozi za Mafunzo ya Hi5



www.jobortunity.org





Kozi za Mafunzo ya Hi5



Jobortunity ni Chuo kinachotoa mafunzo katika maendeleo ya kitaaluma kilichopo Arusha, Tanzania. Kinatoa kwa vijana wenye umri kati ya miaka 18 - 25 ambao wana motisha ya kufanya kazi. Tunatumia mbinu sanifu ya Hi5 kufundishia. Mbinu hii huhakikisha vijana wanakuwa wataalamu jasiri wenye mitazamo chanya, ujuzi wa kijamii na kiufundi ili kukidhi viwango vya soko la ajira Tanzania.

Tunafundisha ujuzi wa karne ya 21 kama vile Mawasiliano, Utatuzi wa migogoro, jinsi ya kuendana na hali ya mabadiliko ushirikiano na Maombi ya Kazi. Jobortunity haitayarishi tu vijana kwa kazi, ila, pia tunatoa msaada wa shirika kwa makampuni. Lengo letu kubwa ni kusaidia vijana kupata ajira hivyo kuboresha maisha yao na pia kwa makampuni kupata wafanyakazi wenye ujuzi na mtazamo sahihi ili kutoa huduma bora.

Tunatoa:

Kozi ya Hi5 ya mwaka mmoja - Kozi hii hufundisha vijana wenye motisha ya kufanya kazi katika sekta ya huduma, kuwa jasiri na wataalamu wenye mitazamo chanya na ujuzi unaohitajika kukabiliana soko la ajira Tanzania. Tunatumia mtaala wetu maalum wa Hi5 uliosanifiwa kwa ushirikiano na makampuni ya hadhi ya juu. Kozi hii ya Hi5 inawainua wanafunzi kujengeka kitaaluma na kimaisha. Wahitimu wetu wanasema: "Hi5 ni ufunguo wa maisha!"

Mtazamo wa kazi

Kazi ambazo wanafunzi watafanya wakati wa mafunzo kwa vitendo na baada ya kuhitimu: Mhudumu wa wageni hotelini, Mpishi, Mapokezi, Mfanya usafi vyumba vya wageni, Mtunza bustani, Mwongoza wageni, Msaidizi wa ofisi kuu, Afisa wa huduma kwa wateja, Mbeba mizigo ya wageni, mesenja.

Ushuhuda wa Mzazi:

Wanafunzi wa Jobortunity huwa na mabadiliko chanya kitabia; tunaona haya kwenye matendo yao hata wakiwa nyumbani.

Kozi ya Hi5 ya mwaka 1 imegawanywa katika Awamu mbili:

Awamu ya 1: Mafunzo ya kina ya miezi 4 kuanzia saa 3 asubuhi mpaka saa 10 jioni, Siku tano (5) kwa wiki hapa Jobortunity. Miezi hii mafunzo yanalenga zaidi kwenye kutumia vidole vitano ili kupata maarifa na mtazamo chanya katika sekta za utoaji huduma.

Awamu ya 2: Baada ya kufanikiwa kumaliza Awamu ya kwanza, wanafunzi wataanza mafunzo ya vitendo kwa muda wa miezi 8 katika kampuni kwenye sekta ya huduma kama vile hoteli. Mafunzo haya hutolewa kwa kushirikiana na wasimamizi wa makampuni na Jobortunity.

Katika kipindi chote cha miezi nane (8) cha mafunzo kwa vitendo waajiri watawafundisha wanafunzi ujuzi wanaohitaji kwa taaluma zao. Kila wiki moja ya mwezi, wanafunzi hurudi Jobortunity kuendelea na mafunzo ya Hi5.

Ujuzi katika Hi5 (Ujuzi wa karne ya 21 unafundishwa kwa masomo yafuatayo:

- Namna ya kujiwakilisha
- Taaluma / ueledi

- Mawasiliano
- Ushirikiano
- Usimamizi wa migogoro na utatuzi wake
- Maendeleo ya mtu binafsi
- Hali halisi ya kazi
- Huduma kwa wateja
- Ujuzi wa kompyuta kwa ajili ya kutafuta kazi
- Mpango: Lengo na welekeo
- Maombi ya kazi
- Stadi za maisha

Baada ya kuhitimu, wanafunzi hupata Cheti cha Hi5. Kisha wanakuwa tayari kukabili kazi kwenye sekta ya huduma. Zaidi ya asilimia 75% ya wahitimu wetu hufanikiwa kupata ajira. Jobortunity hutoa huduma ya kuunganisha wahitimu na kazi zinazowafaa kwenye soko la ajira.

Vigezo vya usahili:

Kiwango cha elimu: Cha chini ni darasa la 7 Cha juu ni kidato cha 4 Pia ajue kusoma, kuandika na kuhesabu.

Gharama za kozi

Gharama za mafunzo ya kozi ya Hi5 kwa sehemu kubwa kwa mwaka mzima, hulipwa na wafadhili wa Jobortunity. Pia makampuni huchangia sehemu ya ada pamoja na kuchukua jukumu la kutoa mafunzo

kwa vitendo kwa wanafunzi. Mwanafunzi huchangia kwa kulipa jumla ya kiasi cha Tsh 585,000/- kwa awamu. Tunaamini kwamba kila kijana ana haki ya kupata fursa ya kusoma na kupata kazi. Endapo mwanafunzi hana uwezo wa kifedha kugharamia malipo ya kozi yetu, tuko tayari kukusaidia kupitia mpango wetu wa ufadhili. Hivyo hata vijana wenye changamoto za kifedha wanakaribishwa Jobortunity.

Nani anaweza kuomba nafasi?

Je una umri kati ya miaka 18-25? Na je unautayari wa kuleta mabadiliko katika maisha yako? Je unafahamu kiingereza kidogo? Basi unakaribishwa kuja kununua fomu ya kujiandikisha (Tsh 5000/-) kisha ushiriki katika usahili. Tembelea tovuti yetu kufahamu siku za usahili au piga simu kwa maelezo zaidi.

Kozi fupi za Hi5

Pia Jobortunity tunatoa kozi za muda mfupi kama vile Kozi ya wiki moja ya inyo husiana na Maombi ya Kazi. Tembelea tovuti yetu kufahamu kozi zetu au piga simu kwa maelezo zaidi.

T: +255 789 975 772/ 682 819 891